# OFISI YA RAIS – TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

## SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BIBI TITI MOHAMED

**MKUU WA SHULE: +255656571076** **S. L. P 45**

**MAKAMU: +255 677436849/+255 765698442** **UTETE/ RUFIJI**

**Telegrams: "BIBI TITI MOHAMED SEKONDARI"**

**E-mail: bibititimohamedisecondaryschoo@gmail.com**

**26/04/2024**

---

**KUMB.NA. ED/BMSS/FV/02………………………………………...**

**MZAZI WA ……………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA BIBI TITI MOHAMED**

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano 2024 katika shule ya Sekondari ya wasichana **BIBI TITI MOHAMED**. Tunampongeza kwa mafanikio hayo. Shule itafunguliwa tarehe **01/07/2024**, Shule ya Sekondari ya wasichana **BIBI TITI MOHAMED** ipo katika Mkoa wa Pwani ,Wilaya ya Rufiji umbali wa kilomita 196, Kutoka Dar- es- salaam. Inapatikana Mji wa **UTETE,** Kitongoji cha **KINDWITWI.** Kwa wanafunzi wanaotoka Mikoa ya kusini (Lindi na Mtwara) washuke Ikwiriri, na wanafunzi wanaotoka Mikoa mingine wafike **DAR-ES-SALAAM - MBAGALA RANGI TATU** stendi mpya, ndipo watapata magari ya moja kwa moja kuelekea **Utete** na Utateremka Shuleni **BIBI TITI MOHAMED**. Mwanao atapokelewa Shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo.

**MUHIMU:** Endapo utachelewa zaidi ya wiki mbili tangu tarehe ya kutangazwa kuripoti Shuleni utakuwa umepoteza nafasi hii.

Ni matumaini yetu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote na Mzazi/Mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.Kama kuna changamoto au maswali yoyote unaweza kupiga simu kwa namba zilizoainishwa hapo juu.

***Tunakukaribisha sana***

**………………………………..**

***LILIAN SHAYO***

**MKUU WA SHULE**

## 1.1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- **SARE ZA SHULE**
  - T-shirt moja rangi ya kijivu yenye nembo ya shule mbele na nyuma
  - T shirt moja ya Arsenal ya njano **yenye nembo ya shule**
  - **Sketi mbili rangi ya kijani jeshi zenye urefu kuvuka magoti mshono wa V.**
  - Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba vya kufunika visiwe na visigino virefu (Jozi 2)
  - Shati nyeupe mbili mikono mirefu /nusu kanzu mbili na hijabu yake kwa wanaotaka (kitambaa cha harua), ziwe na nembo ya shule.
  - Soksi rangi nyeupe jozi 2 au Zaidi
  - Viatu vya michezo na kushindia (raba rangi nyeupe) na **SANDAL** zisizo na urembo.
  - Kandambili kwa ajili ya kuogea tu
  - mtandio/juba rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kushindia kwa wanaovaa hijabu zisizo na urembo.
  - Sweta moja kijani jeshi.
  - Kila mwanafunzi lazima aje na **Tracksuti ya blue.**
  - Sketi blue bahari 2 yenye mshono wa Rinda boksi iwe na urefu kuvuka magoti,na shati la damu ya mzee kwa ajili ya kushindia.

***NB:*** *mwanafunzi atapokelewa endapo atavaa* ***Tracksuti ya blue*** *wakati wa kuripoti, mavazi ya nyumbani hayaruhusiwi kabisa shuleni.*

## 2. MAHITAJI YA BWENI

- Godoro la nchi 4 QFL au DODOMA lenye kava ngumu isiyovujisha maji
- Shuka rangi ya blue Jozi tatu
- Mto na foronya 2 za blue
- Taulo

- Nguo za ndani/chupi Zaidi ya 12 **NA TAULO ZA KIKE** paketi sita.
- Ndoo tatu zenye mifuniko lita 10 ( ndoo 2 kwa matumizi ya mwanafunzi na ndoo 1 kwa matumizi ya jikoni)
- Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili (tranker)
- Vyombo vya chakula, chombo chenye mfuniko alimaarufu kama CONTENA, Kijiko, Chupa ya chai.
- Chandarua futi 3x6 pembe nne.
- Mwamvuli mmoja mdogo, tochi au taa ya kuchaji kwa ajili ya kujisomea umeme unapokata
- Mfuko maarufu unaoitwa SHANGAZI KAJA kwa ajili ya kuhifadhia madaftari.
- NB: Mwanafunzi hatopokelewa kama hatokuwa na Bima ya Afya NHIF au CHF au bima yoyote ya matibabu, kama hana afike na 5000/= kwa ajili ya kulipia bima ya jamii ya CHF.

3. **MAHITAJI YA TAALUMA/DARASANI**

- Rimu 2 kwa mwaka size A4
- Result slip ya kidato cha nne
- Picha sita (passport size) akiwa amevaa shati jeupe na rangi ya blue nyuma ya picha.
- Picha moja kwa kila mzazi/walezi wawili (passport size).
- Cheti cha kuzaliwa halisi na Nakala
- Madaftari ya kutosha kwa ajili ya mchepuo wake (Counter Book), Kalamu Peni/Penseli za kutosha
- Mathematical Sets na scientific calculator (CASIO - FX 991MS ),stop watch.
- Dissection kit kwa ajili ya kujifunzia
- Koti la maabara ( lab coat)
- Faili 2 kwa ajili ya kuhifazia mitihani na kumbukumbu zingine ‘FILE FOLDER’
- Graph pad (Graph papers)
- Begi la kubebea madaftari.

## ORODHA YA VITABU

| S/N | SOMO | AINA YA KITABU |
|---|---|---|
| **1** | BIOLOGY | • BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY FORM FIVE BY TIE<br>• BIOLOGICAL SCIENCE (BS) BY D.J. TAYLOR<br>• UNDERSTANDING BIOLOGY FOR ADVANCED LEVEL BY GRENN AND SUSAN TOOLE<br>• BIOLOGY A FUNCTION APPROACH FOURTH EDITION BY M.B. V.ROBERT<br>• MODERN ABC BIOLOGY CLASS XII PART 1 AND 2 BY DR. B.B.ARORA<br>• S. CHAND'S BIOLOGY FOR CLASS XI &XII BY DR .P.S.VERMA |
| **2** | CHEMISTRY | • GENERAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS<br>• PHYSICAL CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS(TIE)<br>• ORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS (TIE)<br>• INORGANIC CHEMISTRY FOR ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOLS(TIE)<br>• MODERN CHEMISTRY ABC OF CLASS XI PART I AND II BY DR.S.P.JAUHAR<br>• PHYSICAL CHEMISTRY BY CHAND |

| | | |
|---|---|---|
| **3.** | PHYSICS | • PHYSICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE BY TIE<br>• PHYSICS FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FORM SIX BY TIE<br>• UNDERSTANDING PHYSICS PART I BY ODASI<br>• UNDERSTANDING PHYSICS PART II BY ODASI<br>• S .CHAND'S PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XI BY V.K.MEHTA AND ROHIT MEHTA<br>• S .CHAND'S PRINCIPLES OF PHYSICS FOR CLASS XII BY V.K.MEHTA AND ROHIT MEHTA<br>• MODERN ABC OF PHYSICS PART I BY SATISH GUPTA<br>• MODERN ABC OF PHYSICS PART II BY SATISH GUPTA |
| **4** | GEOGRAPHY | • PHYSICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SCHOOLS BY TIE<br>• PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SCHOOLS BY TIE<br>• HUMAN GEOGRAPHY FOR ADVANCED SCHOOLS BY TIE<br>• FUNDAMENTAL GEOGRAPHY BY JOSEPHAT MWITA |
| **5** | BASIC APPLIED MATHEMATICS | • BASIC APPLIED MATHEMATICS BY TIE |

| | | |
|---|---|---|
| | (BAM) | |
| **6** | GENERAL STUDIES | • GENERAL STUDIES BY TIE |

**4. MAHITAJI MENGINE**

**I**

| S/N | TAHASUSI | VIFAA |
|---|---|---|
| 1 | PCB | • Jembe lenye mpini<br>• Rubber squizer<br>• kwanja<br>• Fagio laini (soft bloom) |
| 2 | CBG | • reki<br>• Fagio chelewa<br>• panga<br>• Fagio laini (soft bloom) |

**II. MICHANGO MBALIMBALI**

| **Na** | **FEDHA KWA AJILI YA** | **KIASI KINACHOTAKIWA** | **JINA NA NAMBA YA AKAUNTI(NMB)** |
|---|---|---|---|
| **1.** | Tahadhari | 5,000/= (Hairudishwi) | |
| **2.** | Kitambulisho cha shule | 5,000/= (ilipwe mara moja kwa mwaka) | **BIBI TITI MOHAMED SECONDARY SCHOOL CAPITATION A/C**<br><br>**A/C Na.21310047625** |
| **3.** | Uendeshaji wa shule | 65,000/ | |
| **4.** | nembo | 5,000/= | |
| | JUMLA KUU YA MICHANGO | **80,000/=** | |

## 5. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII, USAFI na TABIA NJEMA kwa ujumla Wanafunzi wanatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima na tabia kauli na vitendo hivyo:

1. Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule au mtu yeyote aliyemzidi umri

2. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu na ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.

3. Hairuhusiwi Kwa mwanafunzi

(a) Kufuga kucha na kusuka nywele hairuhusiwi

(b) Kunyoa kipara

(c) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa

(d) Kuvaa vitu kama mapambo mfano Hereni, Mikufu bangili au vitu vya kiimani kama vile Rozali, Kofia, Kanzu, kwa kuwa Shule hii ni ya Serikali. Kuwa na mafuta au manukato yenye harufu kali.

(e) Kuvaa kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule

(f) Kuvaa sketi chini ya kiuno au Kuvaa nguo za mtindo, mfano- model

4. Mwanafunzi atasimama kwenye mstari wakati wa kupata huduma

5. Mwanafunzi atanyoosha mkono juu na kusimama anapouliza au kujibu swali

6. Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu Kwa wengine anapokuwa Darasani Maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi nk

7. Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule.Hivyo

Mwanafunzi:

A. Aripoti shuleni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.

B. Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa

C. Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa

D. Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki wa uwepo wake shuleni (Roll call). Ukaguzi wa Usafi , kupandisha Bendera ya Taifa na Mikutano ya darasa .

D.Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya Alasiri **(9;30-10:30)** NA usiku kuanzia saa **2;00-5;00** .Siku ya Jumamosi maandalio ya masomo yataanza saa 4 asubuhi hadi saa 7 mchana

8**. NI LAZIMA** mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** kwa nyakati zote awapo

shuleni na nje ya shule.

9. Jumapili ya Mwisho wa mwezi ni siku ya wanafunzi kwenda kupata mahitaji yake muhimu kuanzia

6 mchana hadi saa 8 Mchana. Zingatia muda na haupaswi kwenda sehemu nyingine yeyote bila ruhusa.

10. NI LAZIMA mwanafunzi awe ndani ya mipaka ya shule wakati wote isipokuwa akiruhusiwa kuwa nje

ya mipaka ya shule kwa ruhusa maalumu, anapaswa kuwa na kibali ( GATE PASS) cha

maandishi.(Kilichotolewa na Mkuu wa shule au Mwalimu wa Zamu)

11`. Mwanafunzi haruhusiwi kujipikia chakula bwenini, wala kutumia electrical heater au jiko la aina yoyote pia pasi ya umeme hairuhusiwi aje na Pasi ya mkaa.

12. Hairuhusiwi kufanya mikutano yoyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhutasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

13. USAFI: Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi Kwa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hali ya usafi.

14. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare za shule muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati au T shirt yake. Mavazi ya nyumbani Hayaruhusiwi kabisa.

15. Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama laini, Charger earphone, Ipadi nk.

16. Hairuhusiwi kujihusisha na mikutano ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

17. MAENEO YASIYORUHUSIWA: Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo bila sababu maalumu, Ofisi za shule , Chumba cha wafanyakazi ,Maabara , Jikoni, Nyumba za wafanyakazi ,Vilabu vya pombe ,Majumba ya starehe , Majumba ya kufikia wageni.

18.BWENINI Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi wa kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake pia mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote bwenini wakati wowote, na ni marufuku kupeleka viti , meza na chakula Bwenini.

19. Mwanafunzi hatakiwi kuja na chakula cha aina yoyote kutoka nyumbani.

MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI AU KUSIMAMISHWA SHULE:

1. Wizi

2. Uasherati, ushoga na ulawiti.

3. Ulevi wa aina yoyote

4. Utumiaji wa madawa ya kulevya km vile uvutaji wa sigara,Bangi,Cocaine ,Mirungi,Kubeli nk.

6. Makosa ya jinai

7. Kuoa au kuolewa

8. Kuharibu Kwa makusudi mali ya umma.

9. Kupigana au kumpiga mwingine.

10. Kudharau Bendera ya Taifa

11. Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa shule

12. Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma Kwa namna yoyote

13. Kutoa lugha ya matusi

14. Kumdharau kiongozi wa shule, mwalimu, mfanyakazi na jamii kwa ujumla

15. Kutohudhuria vipindi, kufeli majaribio na mitihani ya mara kwa mara shuleni.

17. Kuwa na simu ya mkononi.

18. Kuwa mchafu kupindukia katika mwili, mavazi na mazingira yanakuzunguuka.

19. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi za kuchana na kitana kidogo ni marufuku kunyoa kiduku, wave, kusuka au kusokota dredi, au rasta na kuvaa wigi

NB: Mzazi umfungulie mwanao akaunti benki ya NMB , shuleni aje na kadi yake. Pesa zote za matumizi yake shuleni ingiza kwenye akaunti yake, Pia huduma ya kufungua akaunti itapatikana wakati akiwa shuleni.

# MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi…………………………………………………….Kidato …….mwaka……

Tarehe ya kuzaliwa……………Kabila la mwanafunzi………………..Uraia wa mwanafunzi…………

Tarehe ya kujiunga na shule hii ………Shule aliyotoka ……………………….…………………

.Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu………………………………………………………..

Je unarudia kidato?……… kwa nini?.........................................................................................

Dini ya mwanafunzi………………… Dhehebu………………………………………..

Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L. P…………Wilaya………………Mkoa………………………

Tarafa………………Kata…………………Kijiji…………………………simu ya nyumbani…………….

Saini ya mwanafunzi……………………………. Tarehe……………………………….

MZAZI/ **MLEZI**

Jina la Baba…….……………………………Kazi ya Baba……..………….Anwani ya sasa……………

Kazi yake……………………………….Dini ya mlezi…………Dhehebu…………

Simu ya nyumbani……………………………na…………....... Saini ya Mzazi/Mlezi…………..

MZAZI/MLEZI

Jina la Mama/Mlezi……………………………………Kazi ya Mama/mlezi…………Anuani…………….

Dini……………………Dhehebu…………………………...Mahali Anapoishi……………………….

NDUGU WENGINE

| Na | JINA | ANWANI | SIMU | UHUSIANO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |

…………………………… UHUSIANO

…………………….. UHUSIANO

…………………. UHUSIANO

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART ‘A’

FROM………………………

TO THE MEDICAL OFFICER ……………………………… ………………………………

Mr./Miss……………………………………………………………………………(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I. Eyesight …………………… Hearing……………………………………………………

Limbs……………………… Speech…………………………………………………………….

Venereal disease………………………………

Leprosy…………………… Epilepsy………………………………………………………….

II . Neuroses…………………………………………………………

III . Other serious diseases ……………………………………………..

IV. Pregnancy…………………………………………………………

Date……………………………………… Signature……………………………………

PART B:

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…………………… (e) Venereal Diseases…………………

(b) Hearing……………………. (f) Leprosy……………………………...

(c) Speech ……………………. (d) Limbs………………………

II Neuroses……………………………

III Other serious diseases……………………………………………………….

……………………………………………………………………………………..

IV .Pregnancy…………………………..

Date……………………………………………Signature……………………………........

Station……………………………………... Designation…………………………

## E. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………………Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI BIBI TITI MOHAMED mwaka …………. ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya BIBI TITI MOHAMED.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.

ii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.

Saini ya mwanafunzi ……………… Tarehe …………

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mim…………………………………ninakubalmtotowangu ………………… Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari BIBI TITI MOHAMED mwaka…..... Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa. Anuani yangu ya kudumu ni ……………………Simu……………… Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/Mlezi ………………………….Tarehe ……………